

RIPOTI YA ZANZIBAR

FinScope

TANZANIA

2023



Ripoti ya Finscope Tanzania ni utafiti wa kina chini ya sekta ya fedha uliolenga watumiaji wa huduma za fedha ambao ni watanzania wenye umri wa miaka kumi na sita (16) na kuendelea. Utafiti huu unatoa uelewa kuhusu kiwango cha matumizi ya huduma za fedha kwa nchi nzima; vile vile ni kipimo sahihi cha uhitaji na matumizi ya huduma za fedha kwa makundi mbalimbali ya watu. Vile vile, uchambuzi unaotokana na ripoti ya Finscope Tanzania unabainisha wazi vikwazo na visababishi/vivezeshi vinavyochangia matumizi ya huduma juumuishi za kifedha. Utafiti ulifanyika kwa ushirikiano baina ya serikali na sekta binafsi, ukiongozwa na Wizara ya Fedha na Mipango kwa Tanzania na Zanzibar pamoja na Benki Kuu ya Tanzania kwa kushirikiana na shirika la Mfuko wa Kuendeleza Sekta ya Fedha Tanzania (FSDT), Ofisi ya Takwimu ya Taifa pamoja na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu Zanzibar.


Ripoti ya Zanzibar inaangazia uchambuzi wa matokeo ya utafiti wa Finscope Tanzania 2023 kwa wakaazi wa Zanzibar. Hii inajumuisha kila mtanzania mwenye umri wa miaka 16 na kuendelea anayeishi Unguja au Pemba ambae wakati wa kukusanya takwimu za utafiti huo aliweza kuchaguliwa kutoa maoni yake kwa njia ya bahati nasibu.

Ripoti ya Finscope ya mwaka 2023 ni awamu ya tano ya mfululizo wa ripoti za Finscope Tanzania ambapo awamu nyingine zilifanyika mwaka 2006, 2009, 2013 na 2017. Ripoti kamili ya Finscope Tanzania 2023 na ripoti ya Zanzibar zinapatikana katika tovuti yetu ya www.fsd.or.tz/finscope/


Hali ya Matumizi ya huduma juumuishi za fedha na maendeleo ya msingi

Matumizi ya huduma juumuishi za fedha yamepiga hatua kwa upande wa Zanzibar. Tangu mwaka 2017, idadi ya watu wazima waliotengwa na huduma juumuishi za fedha imepungua kwa kiasi kikubwa kwa takriban theluthi mbili hadi 112,000 kwa mwaka 2023 kutoka 318,000. Kupungua kwa waliotengwa na huduma juumuishi za fedha kunaonesha tofauti kubwa zaidi kwa sababu idadi ya watu wazima imeongezeka kwa asilimia 27 katika kipindi hicho. Kuongezeka kwa matumizi ya huduma za fedha kwa njia ya simu za mkononi kutoka asilimia 38 hadi asilimia 78 na huduma za kibenki kutoka asilimia 15 hadi asilimia 25 imechangia kwa kiwango kikubwa ukuaji wa huduma juumuishi za kifedha.

Matumizi ya Huduma Rasmi za Fedha Msingi = Zanzibar




Matumizi ya Huduma za Fedha Msingi = Zanzibar



- Wanazo au wanatumia huduma za kibenki
- Hawana au hawatumii huduma za kibenki, ila wanazo au wanatumia huduma nyingine rasmi za fedha
- Hawana au hawatumii huduma rasmi za fedha, ila wanazo au wanatumia huduma za fedha zisio rasmi
- Wametengwa kabisa na huduma rasmi za fedha

Maswala ya Umbali, NIDA na Simu Msingi = Kwa Zanzibar



Vikwazo vya kupata huduma za kifedha vimepungua, ingawa bado ni **changamoto kwa baadhi ya makundi ya watu**




Kwa upande wa Zanzibar, changamoto za kuweza kupata huduma zimetatuliwa kwa kiwango kikubwa kwa kuwa asilimia 100 ya watu wanaishi ndani ya kilomita 5 kutoka kituo au eneo linakopakana huduma za fedha, upatikanaji wa namba ya utambulisho wa kitaifa bado uko juu kwa asilimia 74, umiliki wa simu za mkononi umeongezeka kutoka asilimia 73 hadi asilimia 86, na upatikanaji wa huduma ya mtandao umeongezeka kwa kiasi kikubwa kutoka asilimia 39 hadi asilimia 52 na umiliki wa simu janja umeongezeka kutoka asilimia 24 hadi asilimia 39.

Hata hivyo, kuna mitazamo hasi baina ya watu ambao bado wanafikiria kuwa wanahitaji kuwa na pesa nyingi ili waweze kufungua akaunti ya benki na pia wanafikiri kujiunga na huduma za bima ni kujitabiria mambo mabaya. Kwa kuongezea, uwepo zaidi wa vyanzo vya kipato vya msimu au ambavyo havina ratiba maalum vinapelekea kukosekana kwa uthabiti wa kifedha. Vile vile kukosekana kwa uelewa kuhusu utoaji wa huduma za fedha zinazoendana na sheria ya dini ya Kiislam imekuwa ni kikwazo pia.

Vikwazo na Mipango Ijayo

Zanzibar imefanya maendeleo makubwa kwenye upatikanaji wa huduma za fedha. Mipango zaidi inahitajika kutoka kwa wadau wa sekta za serikali na binafsi ili kuhakikisha kuwa watu wengi zaidi Zanzibar wanafanya miamala kwa njia rasmi na wanatumia huduma za fedha ili kukuza maendeleo ya kiuchumi.

Mapato yako kibinafsi yanapatikana kupitia vyanzo gani na ni mara ngapi pesa hupatikana kutoka kwa vyanzo hivi?




Zaidi ya theluthi ya wahojiwa kutoka Zanzibar wanategemea watu wengine ili kupata kipato

Matumizi ya huduma za malipo kwa njia za kidijitali bado ni ya kiwango kidogo sana



Njia za malipo za wauzaji zinazotumiwa kununua bidhaa

Msingi = Watu wazima Zanzibar




Mwezi uliopita Umewahi tumia

Kutokana na kiwango cha juu cha utegemezi, walioshiriki mahojiano ya utafiti huu kutoka Zanzibar walikuwa aidha wanapokea fedha tu na walikuwa na uwezekano mdogo wa kufanya miamala ya kielektroniki au kwa wale asilimia 21 ambao wengi wao ni wanawake, utegemezi wao ulikuwa ni wa kuletewa bidhaa moja kwa moja na wanakaya wengine. Hii inakwamisha uwezo wao wa kumudu pesa taslim. Hata hivyo, muda mwingine wanajihusisha kwa njia isiyo ya moja kwa moja na mali kauli ambapo inatoa fursa ya kuweza kupata historia yao ya mikopo iliyojitosheleza- hili ni eneo la ubunifu ambalo linatakiwa kufanyiwa tathmini zaidi.

Ingawa wakazi wa Zanzibar wana ufahamu juu ya huduma za malipo kwa njia ya kidijitali mfano Lipa Namba na kifaa cha malipo, ni sehemu ndogo tu ya waliohojiwa wamewahi kutumia huduma hizo na ni wachache zaidi huwa wanazitumia mara kwa mara. Wengi wao wanafanya malipo kwa njia ya pesa taslimu.

Matumizi ya njia za malipo kwa kidijitali sio tu itawezesha uchumi wa kidijitali lakini pia itakuza uchumi na ubunifu na pia kuongeza uelewa juu ya matumizi ya fedha miongoni mwa watu. Hii itawezesha hata wateja ambao wana umiliki mdogo wa mali kuweza kufanyiwa tathmini ya kupata mkopo kwa usalama.



Wahojiwa wengi kutoka Zanzibar wanakopa au kuweka akiba kwa ajili ya kurahisisha mzunguko wa fedha

Uchambuzi wa matokeo ya Zanzibar unaonesha ongezeko la idadi ya watu wanaoweka akiba ambayo inaainisha ongezeko la ufahamu juu ya umuhimu wa kuweka akiba wakati wa hali ngumu. Hii ni kutokana na uzoefu wa hivi karibuni uliosababishwa na janga la dunia la mlipuko wa ugonjwa wa UVIKO-19, ambao uliathiri sekta ya utalii kwa kiasikikubwa kwa kuwa ni shughuli kuu ya kiuchumi Zanzibar.

Hata hivyo, uwekaji akiba na ukopaji bado unafanyika kwa ajili ya kurahisisha mzunguko wa fedha. Changamoto iliyopo ni kuongeza idadi ya wahojiwa kutoka Zanzibar ambao wanatumia fedha kwa ajili ya malengo ya maendeleo kama vile kuongeza mali au kufanya uwekezaji wenye tija ili kuwa na vyanzo tofauti tofauti vya kipato.

Njia za binafsi na kijamii za kukabiliana na majanga zinatumiwa zaidi kuliko bima rasmi, kwa kuwa asilimia 8 tu ya wahojiwa kutoka Zanzibar ndio wana bima. Hata hivyo, sababu nyingine inayopelekea matumizi madogo ya bima ni kutokana na serikali kugharamia matibabu kwa kiwango kikubwa ambayo inapelekea kutokuwa na umuhimu wa kuwa na bima ya afya, hii ni tofauti na upande wa bara.